

NUNGU

KWA

VARWA

Na Dr Catherine BAROIN

Muhtasari

Wameru (*Varwa*), ambao ni jamii ya wakulima wenye asili ya Kibantu na waishio katika maeneo ya Mlima Meru (Kaskazini mwa Tanzania), ni watu wenye kuamini na kuhofia sana nguvu ya laana licha ya juhudi za makanisa katika kukemea imani hiyo. Hofu hiyo inatokana na kuamini matambiko ambayo hutumika kama njia ya kupata suluhu ya migogoro baina ya wana jamii baada ya sheria rasmi za nchi kushindwa kupata ufumbuzi. Tambiko hilo linalojulikana kama 'Kuvunja chungu' ni kwa ajili ya kuacha laana kwa mtu aliyetenda kosa. Kwa hofu ya kupata laana, mara nyingi mkosaji hukiri makosa na kulipa fidia ya makosa aliyosababisha na kisha hufanyika tambiko jingine kwa ajili ya kupoza laana ya tambiko la awali ili isimuathiri mkosajji ambaye tayari amekwishakiri kosa. Kitini hiki kinalenga kueleza sababu na mazingira yaliyosababisha kuanzishwa kwa utaratibu huu, namna unavyotekelezwa na kisha kitajadili sababu za ufanisi wa utaratibu huo.

Matumizi ya matambiko ya laana kama utaratibu wa kutafuta haki katika jamii ya Wameru (*Varwa* kwa Kimeru) waishio Kaskazini mwa Tanzania.¹

Na Dr Catherine BAROIN²

Sheria rasmi za nchini Tanzania na zile za mila katika jamii ya Wameru wa Mlima Meru hazishabihiani licha ya kwamba mara nyingi hufanya kazi kwa ukaribu. Hata misingi ya utendaji kazi wake ni tofauti ambapo sheria rasmi za Tanzania, nyingi zikiwa zimetokana na sheria za kikoloni hulenga kumtia hatiani na kumwadhibu mkosaji wakati zile za kimeru hulenga kupata suluhu na kwamba ili kufikia suluhu hiyo, hatua ya mwisho huwa ni ya kufanya tambiko ili kumwadhibu mkosaji ambaye bado hajajitaja. Andiko hili kitaeleza kwa ufupi juu ya jamii ya Wameru na kisha kueleza namna mifumo hiyo miwili ya sheria (sheria za nchi na zile za mila za Wameru) inavyoingiliana na baadaye kitaeleza juu ya utaratibu wa tambiko la laana ambalo licha ya ushawishi wa dini ya kikristo, utaratibu huo umebaki kuwa njia ya kuaminika katika kutafuta haki katika jamii ya Wameru.

¹ Tafiti hii inajikita zidi katika tafiti zilizofanywa katika eneo husika na mtafiti wa Kitanzania. Utafiti huo ulioanza mwaka 1992 hadi 2010 uligawanywa katika vipindi tofauti sita ambavyo vinafanya jumla ya muda wa utafiti kuwa ni mwaka mmoja na nusu. Angalia pia 'thesis' ya Justin MUNGURE (2002).

² Kitini hiki kimetafsiriwa kwa Kiswahili na Aggrey MEENA kutoka katika kitini cha Kifaransa: Catherine BAROIN, "La malédiction au secours de la justice chez les Rwa de Tanzanie du Nord", R. Verdier, N. Kalnoky & S. Kerneis (eds.), *Les Justices de l'Invisible*, Paris, L'Harmattan, p. 317-330. ISBN : 978-2-343-00437-2-EAN : 9782343004372.

Wameru ni watu gani ?

Wameru ni jamii ya wakulima na wafugaji ambao lugha yao ina asili ya Kibantu. Tangu karne ya 18, jamii hii ambayo idadi yake ni takribani watu 250,000 (takwimu za mwaka 2012) imeanza kuishi pembezoni mwa Mlima Meru (wenye urefu wa mita 4585) katika upande wa Kusini-Mashariki unaotazamana na Mlima Kilimanjaro. Nchini Tanzania hujulikana kama Wameru ingawa katika lugha yao ya kimeru (*ki-rwa*) hujiita *Varwa*. Utamaduni wao na lugha yao vina ukaribu na jamii jirani ya Wachaga waishio pembezoni mwa Mlima Kilimanjaro. Kama ilivyo kwa Wachaga, Wameru pia hulima kahawa (kama zao la biashara), ndizi na mazao mengine ya chakula hususani maharagwe na mahindi. Kwa ajili ya kujiongezea kipato, hujihusisha pia na ufugaji kwa mtindo wa ufugaji wa ndani kwa kuwa eneo hili la mlima lina idadi kubwa ya watu. Kufuatia kuporomoka kwa biashara ya kahawa, mji jirani wa Arusha umegeuka kuwa mkombozi wa Wameru kiuchumi ambapo huuza bidhaa zao za shambani na pia kupata ajira kwa wale wenye ujuzi mbalimbali.

Mwanzoni mwa karne ya 19, Wameru walikuwa chini ya ukoloni wa Wajerumani ambao uliambatana na kuingia taratibu kwa kanisa la Kilutheri. Wakoloni wa Kingereza pia waliendeleza ukuaji wa kanisa la Kilutheri hadi kipindi cha uhuru mwaka 1961. Kwa sasa Wameru walio wengi ni Walutheri na wamepata elimu kwa kiwango cha sekondari na chuo kikuu. Wameru wote huzungumza lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha rasmi na lugha ya taifa Tanzania na

baadhi huzungumza lugha ya Kingereza ambayo pia ni lugha rasmi nchini Tanzania.

Hata hivyo, Wameru bado hawajaacha kufuata mfumo wao wa kijamii wa jadi ambao msingi wake unafuata umri (rika) na utawala wa ukoo na kwamba mamlaka ya juu ipo kwa wazee wa ukoo wa upande wa mwanaume (patrilineal). Licha ya kuwa kila familia inasimamia shughuli zake na mali zake yenyewe, bado familia huwa chini ya uangalizi wa ukoo wa upande wa mwanaume na kwamba wazee wa ukoo huingilia kati pindi patokeapo matatizo mbalimbali kama vile migogoro inayohusu mgawanyo wa urithi hususan ardhi. Masuala ya ardhi ni muhimu sana kutokana na kuwepo kwa upungufu mkubwa unaosababishwa na kuongezeka kwa idadi ya watu. Mfumo wa rika kwa upande wake, unabainisha makundi ambayo huvuka ngazi moja hadi nyingine kwa utaratibu maalum. Mara baada ya kupitia jando, vijana wadogo, ambao hupata ushauri kutoka kwa baba zao, huingia kwanza kundi la vijana (*wasero* kwa Kimeru, *warriors* kwa Kingereza) ambao kwa sasa wanajihusha na baadhi ya kazi za jumuiya. Vijana hawa hufundishwa kuheshimu wakubwa zao kiumri sanjari na kupewa mafunzo yanayohusu mambo ya ndoa ambayo hukataza ndoa baina ya watu wanaotoka kwenye familia zenye uhusiano wa kindugu. Pia mwanaume hukatazwa kuoia binti wa mtu mwingine ambaye wanalingana rika. Kila ukoo na kila kikundi huchagua viongozi wake wa kijadi (washili) pamoja na kiongozi mkuu wa kikundi (Mshili Mkuu). Washili hao kutoka koo mbalimbali huunda Kamati Kuu inayokuwa na wajumbe 20 hadi 30. Kamati hiyo

inaongozwa na Mshili Mkuu (*Nshili nnini* kwa lugha ya kimeru) ambaye anakuwa na ofisi yenye watendaji kati ya wane hadi watano akiwemo katibu na mtunza hazina. Kamati Kuu chini ya Mshili Mkuu ina jukumu la kusimamia taratibu zote za jamii kwa kufuata Katiba ya Wameru. Katiba hiyo ya maandishi ambayo inaainisha sheria za mila ni ya kipekee nchini Tanzania³ na hufanyiwa mabadiliko kulingana na mabadiliko ya sheria rasmi za nchi.

Sheria rasmi za nchi na zile za kimila

Wameru pamoja na kufuata tamaduni zake za asili, huchangamana vema na jamii nyingine nchini Tanzania. Wameru kadhaa wakiwemo wafanyakazi na wanasisia wanashiriki kikamilifu katika shughuli za utawala nchini. Wameru hushiriki kwa hamasa katika masuala ya kiraia kama vile chaguzi mbalimbali za nchi, iwe za serikali ya mtaa au uchaguzi mkuu. Jamii hii hauoni mfumo wake wa sheria za mila kama mfumo pinzani dhidi ya sheria rasmi za nchi bali kama nyongeza katika sheria hizo rasmi ambazo msingi wake unatokana na sheria za kikoloni (za Magharibi). Mfumo huo wa sheria rasmi za nchi unahusisha mahakama za ngazi tofauti huku Mahakama ya Rufaa ikiwa ndiyo yenye mamlaka ya juu zaidi. Mifumo hii miwili inafanya kazi kwa pamoja licha ya kuwa na misingi na historia tofauti kabisa. Kama ilivyo mifumo ya sheria ya nchi za Magharibi, mfumo rasmi wa sheria za Tanzania unalenga kumtambua na kumwadhibu mkosaji na pia ni aghali. Aidha kwa maoni ya Wameru, mfumo wa sheria za nchi siyo kwamba tu ni

³ BAROIN, 2003

aghali bali una urasimu na huusisha sana vitendo vya rushwa kiasi kwamba mara nyingi utoaji wa hongo ndo unaoamua upatikani wa haki. Faida za mfumo huo ni kuwa unazo njia za kulazimisha utekelezaji wa sheria kama vile magereza, utozaji wa faini na uzuiaji wa mali. Kwa upande wa mfumo wa sheria za kijadi, zenyewe siyo ghali, hakuna vitendo vya rushwa ama kama vipo ni kidogo. Hata hivyo mfumo huo hauna njia za kulazimisha utekelezaji wa sheria zake zaidi ya kutegemea nguvu ya jamii katika kukemea makosa husika ama kutegemea laana inayotokana na imani za jadi.

Mambo matatu huweza kutokea. Kwa suala la uhalifu mdogo, mlalamikaji anaweza akashitaki moja kwa moja katika mahakama za serikali lakini ukoo husika ukaona kuwa ni vyema suala hilo likasuluhishwa na wanaukoo wenyewe na hivyo kuepuka gharama kubwa, utaratibu ambao umeonekana kuwa madhubuti. Hivyo mshili wa ukoo humwomba hakimumu wa serikali amuachie shauri hilo. Kwa kawaida hakimumu hukubali lakini huupa ukoo muda maalumu wa kuhakikisha kuwa shauri hilo limepatiwa suluhu. Wakati mwingine hakimumu wa serikali anapokabiliwa na ugumu wa katika kupata ufumbuzi wa shauri flani huomba msaada kwa wahusika wa sheria za mila. Ukoo au koo husika hutafakari shauri hilo na kisha hukabidhi kwa hakimumu wa serikali, ripoti ya maandishi ikiwa imetiwa saini na muhuri na mshili/washili wa ukoo/koo. Jambo la tatu linaloweza kutokea ni pale sheria za nchi zinapotoa hukumu kimakosa kwa kuzidiwa umakini na mhalifu. Upande ulioshindwa huamua kupeleka shauri katika taratibu za kimila. Ili kupata haki, upande wa walalamikaji huomba kufanyika kwa

tambiko la kuacha laana linalojulikana kama ‘vunja chungu’ (*ibara nungu* kwa Kimeru). Tambiko hilo haliwezi kufanyika bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa ungozi wa jadi.

Tambiko la ‘kuvunja chungu’: utangulizi

Tambiko hili la kisheria humsababishia mkosaji laana iitwayo *kidengo* kwa Kimeru. Laana hii ni moja ya aina tatu za laana kwa Wameru. Kitini hiki hakitazungumzia aina hizo nyingine mbili. Laana ya *kidengo* haitokani tu na tambiko bali hata kwa kauli tu za wazazi au ndugu wa karibu ambao watahisi kutotendewa haki na ndugu mwingine. Tofauti na laana nyingine, laana ya *kidengo* inaweza kufutwa kwa tambiko jingine maalumu na hivyo kuondosha athari zake kwa mlengwa.

Tambiko la ‘kuvunja chungu’ ni tendo la wazi⁴ ambalo lengo lake ni kuacha laana kwa mkosaji ambaye bado hajakiri kosa au bado hajafahamika. Kwa lugha ya Kimeru tambiko hili hufahamika kwa jina la *ibara nungu* ikiwa na maana ya kuvunja chungu kwa Kiswahili. Tambiko la aina hiyo hufanyika pia katika jamii nyingine za Kaskazini mwa Tanzania (Wamasai, Waarusha, Wachaga⁵, Wapare n.k) isipokuwa katika namna tofauti tofauti. Kitini hiki kinazungumzia tambiko linalofanywa na jamii ya Wameru pekee, tambiko ambalo lengo lake ni kumpa mkosaji (ambaye bado hajafahamika) chaguzi zifuatazo: aidha ajitaje (ambapo atatakiwa kumaliza tatizo au kulipa faini ya kosa) ama ajiingize yeye na ndugu zake katika laana. Ufanisi wa tambiko hili unatokana na ukweli

⁴ Mara chache huweza kufanywa kwa siri

⁵ Angalia Wilhelm MOHLIG, 1991

kwamba Wameru karibu wote bado wana imani kubwa kuwa laana hiyo ina athari kubwa licha ya juhudi za Mekanisa za kupinga uwepo wa nguvu ya laana hiyo.

Kufanyika kwa tambiko

Mlalamikaji hutakiwa kuwa na sababu za msingi za kutaka kufanyika kwa tambiko hilo. Sababu zinaweza kuwa ni kuibiwa, kusogezwa kisirisiri kwa mpaka wa shamba⁶, kuharibiwa kwa mali, kudhuriwa mwili au kuuawa kwa ndugu na kwamba muhusika wake hajafahamika bado. Mlalamikaji anaweza kuwa pia hakuridhishwa na hukumu katika mahakama ya serikali ambayo ilimpa ushindi mshitakiwa. Athari za tambiko la chungu siyo za kubeza kwani huweza kusababisha:

- kifo kwa mkosaji mwenyewe, wazazi wake, watoto wake (wale aliowazaa yeye), ndugu zake wa ukoo mmoja,
- kuzaliwa kwa mtoto mwenye ulemavu,
- ugumba (kwa binadamu au wanyama)
- mavuno hafifu ya mazao,
- magonjwa katika familia au
- ugonjwa wa akili,
- ajali za mara kwa mara za aina mbalimbali,
- umasikini ambao wakati mwingine unaweza kusababisha ufukara kabisa.

⁶ Kutokana na ukuaji wa idadi ya watu, ardhi imekuwa haba na kusababisha ongezeko maradufu la migogoro ya ardhi.

Kwa jumla, laana hulenga kuathiri uzazi na mafanikio ya mhalifu pamoja na ndugu zake. Mfululizo wa majanga yanayotokana na laana hii huathiri familia ya mkosaji, wakati mwingine hata miaka mingi baadae na bila ukomo wa muda. Wameru wanathibitisha kuwa kwa kawaida ni wanaukoo ndiyo huathirika kwanza hata kabla ya mkosaji mwenyewe ambaye anaweza kuathiriwa wa mwisho na laana ambayo ilimlenga yeye. Wanawake kwa upande wao, huamua kuzaa na mwanaume wa ukoo mwingine ili kuepuka laana hiyo kwa imani kwamba angalau baadhi ya watoto wake watasalimika na laana endapo itawapata wanaukoo wa mume wake.

Kutokana na kuwa na athari kubwa, tambiko la ‘kuvunja chungu’ hufanywa kwa kufuata taratibu kali ambapo huitaji vibali mbalimbali kutoka kwa mamlaka rasmi. Kwanza ni ukoo wa mlalamikaji ndiyo unaotakiwa kukubali kufanyika kwa tambiko. Wanaukoo hujadili juu ya kufanyika kwa tambiko husika kwa kuwa ni wao ndiyo watakaokuwa wa kwanza kuathirika endapo mkosaji (ambaye bado hajajulikana) atakuwa ni miongoni mwao na hivyo laana ya tambiko kuwarudia wao, jambo ambalo limeshawahi kutokea. Kwa hiyo, ukoo hufanya uchunguzi wake kwanza na kuhakikisha kuwa mkosaji si mmoja wa wanaukoo wao na kisha kuruhusu kufanyika kwa tambiko ambapo mshili wa ukoo huwasiliana na Kamati Kuu ya Wameru ili kumpa kibali cha kufanya tambiko hilo. Kamati Kuu ambayo inaundwa na washili wa koo na viongozi wa makundi rika chini ya uongozi wa Mshili Mkuu hushauriana juu ya ombi hilo. Endapo Kamati Kuu itaridhia huarifu

ukoo husika kwa kibali cha maandishi kilichopigwa muhuri⁷. Baada ya kibali hicho, suala hilo hufikishwa kwa Afisa Mtendaji wa serikali za mtaa, ambaye ni mtendaji aliye chini ya sheria rasmi za Tanzania. Naye pia hutoa kibali kwa maandishi. Mara baada ya kupata vibali hivyo, mlalamikaji humtafuta mtaalam wa tambiko na kumwomba kufanya tambiko hilo.

Mtaalamu wa tambiko la ‘kuvunja chungu’ na chungu chake

Kwas sasa, wataalamu wa tambiko la ‘kuvunja chungu’ wamekuwa wachache na wengi wao wamezeeka. Wengi wao wameacha kazi hiyo baada ya kuingia katika Ukristo, sababu ambayo inaongeza ugumu katika kuwapata wataalam wapya kwa kuwa baada ya kuingia katika ukristo, wazee hao hawapo tayari tena kutoa ujuzi wao kwa wataalamu wapya. Aidha ni wanaume pekee ndiyo wanaweza kuwa wataalamu wa tambiko hilo na kamwe si wanawake. Kikawaida katika jamii ya Wameru, wanawake huwa hawajihusishi na masuala ya matambiko wala siasa, lakini sasa wapo wana siasa.

Vilevile ni kawaida kukuta mtaalamu wa tambiko akiwa na kasoro kimwili: mlemavu, kiwete au chongo na Wameru wanazona kasoro hizo kama sifa muhimu katika kuwasiliana na nguvu za asili (supernatural power). Hata hivyo sifa hizo haziwiani na nguvu za asili kwa kuwa mshili hatarajiwi kuwa na kasoro za kimwili na hivyo mfanya tambiko hawezi kuwa mshili.

⁷ Angalia chapisho la Tim KELSALL,2003, uk.185.

Ujuzi wa tambiko hurithishwa kutoka kwa baba kwenda mtoto lakini ni mtoto mwenye kuchukua jina la ukoo wa baba pekee ndiye anaweza kurithishwa ujuzi huo. Katika jamii ya Wameru, watoto wa kiume, kulingana na nafasi zao za kuzaliwa, hupewa majina kutoka kwenye ukoo wa upande wa baba na ule wa upande wa mama. Hivyo ni watoto wa kiume waliozaliwa katika nafasi isiyogawanyika kwa mbili (waliochukua majina ya ukoo wa baba) ndiyo wanaweza kurithi ujuzi wa baba zao katika kufanya tambiko la ‘kuvunja chungu’.

Mbali na kufuata urithi katika familia, mtu mwingine yeyote huweza kuamua kuwa mfanya tambiko baada ya kuathiriwa na laana. Kwa mfano, mmoja wa Wameru ambaye alizaliwa mwaka 1910, aliamua kuwa mtaalamu wa tambiko la ‘kuvunja chungu’ baada ya watoto wake sita kufariki kwa mfululizo. Lengo lake la kwanza lilikuwa ni kulipiza kisasi kwa vifo hivo vya watoto wake, vifo ambavyo alivitilia mashaka. Alipata ujuzi huo kutoka kwa Wapare, jamii ambayo inaishi katika Mlima Pare iliyopo umbali wa kilomita 150 kutoka Mlima Meru upande wa Kusini-Mashariki. Alipata ujuzi wa namna ya kufanya tambiko pamoja na chungu chake kutoka kwa Wapare ambao wanasifika kwa kuwa na ujuzi huo na kisha akarejea kijijini kwake kama mtaalamu wa kufanya tambiko hilo. Baadae aliachana na kazi hiyo baada ya kuwa mkatoliki.

Ifahamike kuwa, siku zote mfanya tambiko, licha ya kulipwa kila anapofanya tambiko, hajawahi kupata utajiri. Inaonekana kama vile utajiri hauwiani na kazi hiyo kwani kwa kawaida mtaalam wa

tambiko huishi katika nyumba ndogo. Kuhusu chungu chake, kamwe chungu hicho hakitunzi ndani kwake anapoishi na badala yake hukificha mahali nje karibu na nyumba yake.

Kimsingi 'chungu' hicho ambacho ni kifaa cha tambiko siyo chombo cha kuweza kuhifadhi kitu bali ni sanamu ndogo ya udongo yenye urefu wa takribani sentimeta 10 hadi 15. Sanamu hiyo huwakilisha mwanaume au mwanamke ambaye anaonekana hana mikono wala miguu. Ni kichwa pamoja na sehemu za kuonyesha jinsia tu ndizo zinazonyeshwa. Sehemu hizo ni matiti na uke kwa upande wa mwanamke (Tazama picha hapa chini)⁸



Kilelezo namba 1, mchoro ambao umetokana na picha iliyochapishwa na Raimo Harjula 1980, uk. 117

⁸ Picha nyingine ya chungu iliyochapishwa na Tim KELSALL (2003, uk.178) inaonyesha sanamu ya kiasili zaidi ikiwa imetengenezwa kwa jiwe la volcano badala ya udongo wa mfinyazi. Sanamu hiyo ni ya jamii ya Wamasai.

Vyungu vya kike vinasifika kwa kuwa na athari zaidi kuliko vyungu vya kiume. Chungu hicho (sanamu hiyo) kinaweza kurithishwa ingawa kinaweza pia kununuliwa kama ilivyokuwa kwa mmoja wa Wameru aliyepata ujuzi pamoja na chungu kutoka kwa Wapare. Pia chungu hicho kinaweza kukodiwa kutoka kwa mtaalamu mwingine. Mmiliki wa chungu hukitunza vyema chungu chake ambapo wakati hakitumii, hukihifadhi kwa bahasha kadhaa dhidi ya dhoruba yoyote. Mbali tu na kuvunjika, mmiliki huchukua tahadhari muhimu dhidi hata ya kupata nyufa. Inapofikia wakati wa tambiko lenyewe, chungu hicho ambacho si chungu hasa bali ni sanamu ya chungu huwa ‘hakivunjwi’ kama inavyoelezwa isipokuwa mmiliki wa chungu hutembea nacho katika sehemu za wazi akiwa amekishika kwa mkono wake wa kulia huku akitamka laana dhidi ya mkosaji. Sasa basi kwanini tambiko hilo liitwe ‘kuvunja chungu’ ?

Jina la tambiko, ‘kuvunja chungu’

Maneno ya Kiswahili na Kimeru yanayotumika kuunda jina hili la tambiko ni kitenzi ‘vunja’ ama *ibara* na nomino ‘chungu’ ama *nungu* na hivyo kupata jina la *ibara nungu* kwa lugha ya Kimeru na ‘kuvunja chungu’ kwa Kiswahili. Tukirejea maana ya meneno hayo, nomino *nungu* kwa Kimeru haina maana ya hiyo sanamu pekee bali pia chungu kikubwa (kinachoweza kuhifadhi kati ya lita 20 hadi 100 za kimiminika) ambacho kinaweza kutumika kuhifadhi chakula au pombe ya jadi inayotokana na ndizi. Tafsiri hii ya kuvunja chungu kwa Varwa inatokana na kitendawili :

- Nijivunje kama chungu au kama kibuyu ?

- Kama kibuyu kwa kuwa kinaweza kuungwa tena

Wanaeleza kwamba kibuyu kikivunjika kinaweza kuungwa upya na kuendelea kutumiwa kwa matumizi mengine wakati ambapo chungu kikivunjika hakiwezi kutengenezwa tena.

Hivyo ni maana ya kutotengenezeka tena ndiyo inayotoa tafsiri ya kuvunja chungu. Wameru huihusisha maana hiyo moja kwa moja na kifo. Uhusiano baina ya kifo na kuvunja chungu unaonyeshwa vyema katika hekaya ya kimeru ambayo inaeleza chanzo cha binadamu kufa. Hekaya hiyo ambayo ilikutwa na kuchapishwa na wamisionari wa Kijerumani katika kitabu kidogo katika lugha ya Kimeru ⁹ ndiyo mwanzo wa kitendawili ambacho ndicho kimechukua nafasi kuu katika maana ya tafsiri ya kuvunja chungu. Kwa ufupi, hadithi hiyo ni kama ifuatavyo :

Hapo zamani watu walikuwa hawafi bali hubadilika tu ngozi na kurudi kuwa vijana. Siku moja, mwanamke mmoja mzee alimtuma binti yake kwenda kuteka maji ili yeye aweze kujibadilisha na kurudi kuwa kijana bila ya binti yake kushuhudia. Binti akaenda kuteka maji lakini chombo alichokuwa akikijaza maji nyumbani kilikuwa kimetoboka na hivyo kila arudipo kutoka kisimani alikuta chombo hicho kikiwa kitupu. Ilipofika mara ya tano alikasirika na kukataa kurudi tena kuteka maji. Akaenda jikoni ambapo alimkuta mama yake amekwishaanza kujibadilisha na tayari alikuwa kashabadilika kuanzia sehyemu ya kichwa hadi kiunoni. Mama yake akamwambia ‘unaona unanisumbua, nimekutuma ukateke maji umekataa, sasa

⁹ EVANGELISCH-LUTHERISCHE MISSION zu LEIPZIG (Ed.) 1931, p.52-53.

nijivunje kama chungu au kama kibuyu?’ Binti yake akamjibu ‘Jivunje kama chungu’. Yule mama akaanguka na kuvunjika vipande kama chungu. Tangu hapo binadamu wakawa wanakufa kwasababu ya binti aliyemwambia mama yake ajivunje kama chungu. Kama angelikuwa amemwambia ajivunje kama kibuyu basi binadamu wasingekuwa wanakufa kwa kuwa wangukuwa wanaweza kuungika na kuendelea kuishi kama jinsi kibuyu kinavyoweza kuungwa na kuendelea kutumiwa.

Kama vile jinsi Wafaransa wanavyotafsiri usemi ‘kuvunja kiko’ (*casser sa pipe* kwa Kifaransa) ndivyo hivyo Wameru wanavyohusianisha tafsiri ya kifo na namna tambiko linavyofanyika. Tuangalie sasa namna tambiko linavyofanywa.

Namna tambiko linavyofanywa

Pindi anapokwenda kuonana na mtaalamu wa tambiko, mlalamikaji anatakiwa awe tayari kufanya suluhu na mkosaji endapo mkosaji atakiri kosa. Mlalamikaji anatakiwa pia awe amehakikisha kuwa mkosaji si mmoja wa wana ukoo wake ili laana ya tambiko isije ikawarudia ndugu wa ukoo wake. Endapo akiwa ana mashaka juu ya mkosaji halisi na hivyo kutaka kuwakinga wazazi dhidi ya laana, mlalamikaji anaweza kufanya tambiko dogo kwanza ambalo linahusisha kupaka mafuta ya kondoo dume kwenye mlango wa nyumba yake kabla na wakati wa kuvunja chungu.

Mlalamikaji, akiwa na vibali husika, huenda kwa mtaalamu wa tambiko na kumweleza sababu za kutaka kufanywa kwa tambiko hilo. Sababu hizo zinatakiwa kuwa na mantiki kwa kuwa mtaalamu

anayo haki ya kukataa kufanya tambiko. Mlalamikaji humlipa mataalamu kiasi cha shilingi 50,000 (mwaka 2010) au kutoa mbuzi ama kondoo kati ya mmoja hadi wawili au ng'ombe mmoja kwa ajili ya tendo hilo la tambiko. Gharama hizo huenda zikaonekana ziko juu lakini Wameru wanaamini kuwa utaratibu huo ni wa gharama nafuu ukilinganishwa na gharama za mfumo rasmi wa sheria za nchi hususani kutokana na kuwepo kwa tatizo la rushwa.

Baada ya mlalamikaji kukubalina na mtaalamu, hatua muhimu inayofuata ni kutangaza tambiko. Tangazo la tambiko hutolewa mwezi mmoja kabla. Kibali cha Kamati Kuu (rejea hapo juu) cha maandishi ya kuchapwa, kikiwa kimepigwa muhuri na kutiwa saini hubandikwa katika miti karibu yote barabarani na kwenye njia panda za eneo zima la Meru. Tangazo hilo hubainisha jina la mtu aliyetaka kufanyika kwa tambiko, sababu za kufanyika na tarehe ya kufanyika kwa tambiko.

Mara nyingi tangazo la tambiko huamsha hofu kwa mkosaji na hivyo mkosaji huamua kujitaja na kumlipa mlalamikaji gharama alizotumia katika mchakato wa kutaka kufanya tambiko na pia, kwa msaada wa wanaukoo wake, humlipa mlalamikaji fidia kwa kosa alilofanya. Pande hizo mbili hufikia muafaka na hivyo kusuluhusha tatizo kwa njia ya maelewano. Hata hivyo tambiko hufanywa kama lilivyopangwa (mwezi mmoja baada ya tangazo).

Alfajiri na mapema, mtaalam hutoa chungu chake kwenye hifadhi na kunyunyizia maziwa katika maeneo ya karibu kama sadaka kwa mizimu (*irasa varumu*) huku akiwa na jani la *isaale* (*Dracaena*) ambalo ni alama ya amani. Msafara huundwa ambapo mtu yeyote

anaruhusiwa kujiunga na kuelekea katika eneo ambalo mlalamikaji anadhani ndipo kosa lilipofanyikia na hivyo ndipo mahali litakapofanyika tambiko. Wakifika katika eneo husika, mtalaamu hujitambulisha kwanza kwa uongozi wa kijiji na kisha huelezea laana inayoenda kufanywa na kwamba endapo anadanganya basi laana hiyo imrudie mlalamikaji mwenyewe.

Baada ya hapo, mtaalamu hutoa ishara ya kuanza kwa tambiko na tambiko hufanyika huku wakitazama upande utakaopendekezwa na mlalamikaji. Mara nyingi upande huo huwa ni ule ambao mlalamikaji anadhani ndipo mkosaji alipoelekea. Katika hatua hiyo, mvunja chungu hatamki kitu kingine chochote zaidi ya laana ambayo huitamka akitembea njia nzima na huku chungu chake kikiwa kwenye mkono wake wa kulia na kukielekeza pande zote nne za njia. Matamko hayo ya laana hayamlengi mkosaji pekee bali hata mashahidi ambao walishuhudia kutendeka kwa kosa na wakanyamaza kimya bila kumfichua mkosaji. Tambiko hufanyika taratibu na huchukua kati ya saa 3 hadi 6 kwa siku na hufanyika kwa siku 3 hadi 7 mfululizo. Mwisho wa tambiko huwa ni kupata chakula cha pamoja nyumbani kwa mlalamikaji aliyeomba kufanyika kwa tambiko.

Chakula kinacholiwa siku hiyo huwa ni chakula cha asili kiitwacho *nswa* ambacho Wameru hukiona ni moja ya alama yao ya utambulisho. *Nswa* hupikwa na mahindi yaliyokobolewa na ambayo huchemshwa katika maji kwa muda mrefu na kisha huwekwa vipande vya ndizi na mwishoni kikikaribia kuiva huwekwa maziwa. Chakula hicho huweza pia kuwekwa maharagwe ambayo

huwekwa kabla ya kuweka ndizi kwa kuwa huchukua muda mrefu zaidi kuiva.

Tambiko la kufuta laana

Baada ya kufanyika kwa tambiko, kila mmoja husubiri kuona laana iliyotamkwa ikitoa athari kwa walengwa, iwe ni mapema au kwa kuchelewa kwa kuwa hakuna ukomo wa muda kwa athari hizo kuanza kuwapata walengwa. Mara nyingi kila athari au matokeo ya laana iliyotamkwa huweza kutokea moja baada ya nyingine katika kipindi cha miaka mingi tangu kutokea kwa athari moja. Ili kuepuka athari hizo, mara nyingi mkosaji hujitaja, iwe ni mara moja baada ya tambiko au miaka mingi baada ya tambiko. Mkosaji hutakiwa kulipa fidia za kosa alilofanya, kurudisha gharama za tambiko alizoingia mlalamikaji pamoja na kugharamia tambiko la kufuta laana.

Wakati mwingine hutokea kwamba laana haikuwahi kufutwa au tambiko la kuifuta likaja kuombwa na wanaukoo wa mkosaji miaka mingi baadaye na wakati mwingine hata baada ya mkosaji kufariki. Katika hali hiyo, jambo linalotokea ni hili lifuatalo. Kwamba katika kipindi cha miaka kadhaa, wanaukoo huweza kuona kuwa ukoo wao unakumbwa na mfululizo wa majanga na hivyo kuamua kutafuta chanzo cha majanga hayo kwa kumwona mganga wa jadi. Uchunguzi wa mganga unaweza kuonyesha kuwa majanga hayo yanatokana na kosa ambalo lilifanywa na mmoja wa mwanaukoo mwezao hapo nyuma na hivyo ukoo humpa mganga kazi ya kumaliza tatizo hilo ili lisiendelee kuathiri ukoo.

Kwa hiyo tambiko la kufuta laana linaandaliwa na hufanyika katika ngazi tatu : Kwanza ni kwa mkosaji mwenyewe au mmoja wa ndugu wa ukoo wa mkosaji kukiri kosa, pili ni kufuta laana na tatu ni maelewano baina ya upande wa mkosaji na ule wa mlalamikaji. Mkosaji, akiwa amesindikizwa na mshili wa ukoo wake, huenda kumwona mlalamikaji aliyeomba kufanyika kwa tambiko la laana na kukiri kufanya kosa. Humpa mlalamikaji kondoo mmoja na pipa (lenye ujazo wa takriban lita 18) la pombe ya jadi iliyotengenezwa na ndizi na kisha kukubaliana siku ya kwenda kwa mtaalamu wa tambiko ili kufuta laana ya tambiko la awali.

Shughuli hiyo huitwa ‘kupoza chungu’ (*yorisa nungu*) na hutakiwa kufanywa kwa kutumia chungu kilekile ambacho kilitumika kuacha laana kwa mkosaji. Hata hivyo kukipata chungu kilekile kilichotumika kutoa laana siyo kazi rahisi kwa kuwa wakati mwingine tambiko husika huwa limefanyika miaka mingi iliyopita. Mkosaji humpelekea mtaalamu wa tambiko kondoo dume mmoja na madebe mawili ya pombe ambapo kondoo huchinjwa na mafuta yake huchemshwa na kuwekwa katika kikombe kidogo. Mtaalamu huenda kuchukua chungu chake na kunyunyizia maziwa kidogo na kisha hurudi kukaa katikati ya watu waliohudhuria tambiko huku akiwa ameshika chungu chake kwa mikono miwili na huku kikiwa bado kimehifadhiwa katika bahasha. Kiongozi wa ukoo wa mkosaji akiwa na kikombe chenye mafuta ya kondoo, hukiri kosa lililofanywa na mwanaukoo mwenzake na kuomba radhi. Mtaalamu huongeza maneno machache na kisha hukipaka chungu mafuta ya kondoo na kuyatawanya mengine pembeni. Mafuta hayo ya

kondoo ni chakula cha mizimu ambao huleta maelewano na amani kwa wanadamu. Baada ya hapo, nyama ya kondoo huliwa na watu wote pamoja na kunywa pombe.

Shughuli hiyo hufuatiliwa na kikao baina ya koo mbili (ukoo wa mkosaji na wa mlalamikaji) kwa ajili ya kufanya suluhu ya mwisho ambapo hujadili juu ya fidia ya kosa lilifanywa pamoja na gharama ya tambiko la awali. Ukoo wa mkosaji huchangishana na kulipa gharama hizo katika utaratibu na kipindi ambacho wamekubaliana na ukoo wa mlalamikaji. Baada ya muda kidogo hufanyika mlo wa pamoja nyumbani kwa mkosaji kama ishara ya kuridhia maelewano ambapo mbuzi au ng'ombe huchinjwa kwa ajili ya mlo huo na pombe ya ndizi hutengenezwa na koo zote mbili. Watu hula na kunywa pamoja na kushikana mikono kama ishara ya maelewano.

Ufanisi wa tambiko

Tambiko la kuvunja chungu bado ni maarufu sana kwa Wameru hadi sasa hivi kwani husaidia kutatua mizozo mbalimbali. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka mmoja, kuanzia mwezi Mei 2001 hadi Mei 2002, jumla ya matambiko 15 yamefanyika chini ya kibali rasmi.¹⁰ Umaarufu huo wa tambiko unapingana na juhudi za Makanisa, mengi yakiwa Makanisa ya kiprotestanti ambayo yanapinga imani za mizimu. Kwa muktadha huo, swali la kujiuliza ni kwanini Wameru wanaendelea kuamini utaratibu huo.

Inaonekana kuwa, sababu kubwa zinajikita katika ufanisi wa tambiko hilo kijamii na kiishara. Sifa yake kubwa ya kwanza ni

¹⁰ Tim KELSALL, 2003, p.186.

kuaminika kwake kwa kuwa tambiko hilo halitoi mwanya wa kufanyika makosa kwa vile ni mkosaji na ukoo wake ndiyo watakoadhibiwa na nguvu za mizimu. Sifa hiyo ni tofauti na hali ilivyo katika mfumo wa sheria rasmi za nchi kwani kwa kuwa husimamiwa na binadamu wenyewe na kukithiri kwa vitendo vya rushwa, hukumu huweza kutolewa kimakosa bila kuzingatia haki wakati tambiko la ‘kuvunja chungu’ halikosei. Aidha, kauli ya kwanza ya mtaalamu wa tambiko ni kutamka laana na kwamba endapo anachoongea siyo kweli basi laana hiyo imrudie mlalamikaji mwenyewe. Mlengwa wa laana huwa siyo rahisi kuonewa kwa kuwa hata tambiko lenyewe huuomba laana hiyo kutoka kwa nuvu za asili zisizo za kibinadamu. Hivyo mizimu ndiyo wenye dhamna ya kutoa ama kutotoa laana husika.

Kuaminika huko kwa tambiko la ‘kuvunja chungu’ kunaleta amani miongoni mwa watu, siyo tu kwa vile wanajua kuwa ni mkosaji na ndugu zake tu ndiyo watakoathirika na laana bali pia kwa vile kwa kawaida hutoa maelezo kwa mkosaji. Hata hivyo, wacosaji ama wahalifu katika jamii ya Wameru kama ilivyo katika jamii nyingine, huwa ni wengi na wenye ujanja mwingi wa kushinda tuhuma dhidi yao. Mwanzoni, na kwa haraka haraka inaweza kuonekana kama ni suala la kubahatisha, lisilo la haki na kwamba hata adhabu yake huwa imekuzwa. Lakini laana humsaidia mtu aliyefanyiwa kosa kwa kuwa hutoa majibu juu ya kile kinachodhaniwa ni suala la kubahatisha. Aidha tambiko hilo huenda mbali zaidi na kutoa majibu ya kina kuliko tu kile kinachoonekana kwa juu juu katika matukio mabaya. Kwa mfano, huweza kutokea ajali ya gari ambayo

imesababishwa na ulevi wa dereva lakini swali la kujiuliza ni kwanini mtu flani ndiyo awe mhanga wa ajali hiyo na kwanini siku hiyo na mahali hapo? Laana ya ‘kuvunja chungu’ ndiyo huweza kutoa majibu juu ya maswali hayo. Katika suala hilo, hoja ya Wameru, ambayo ina mantiki, hufanana na ile ya jamii ya Waazandé waishio Afrika ya Kati. Hoja hiyo ilichambuliwa na E.E. Evans-Pritchard¹¹. Kutokana na uhusiano wa kimantiki baina ya laana na matukio mabaya, laana huimarisha utulivu wa kiishara duniani.

Zaidi ya yote, tambiko la ‘kuvunja chungu’ lina faida moja kubwa ambayo ni kwamba mara nyingi hutoa mwanya wa kumaliza tatizo kwa kufanya maridhiano. Maridhiano hayo huweza kufanyika kwa kulipa faini baada ya mkosaji kukiri kosa na kisha kufanyika kwa tambiko la kupoza laana ya awali. Pande hizo hupata chakula pamoja na kushikana mikono. Lakini hata kabla ya hapo, tambiko lenyewe la ‘kuvunja chungu’ humfanya mkosaji kukiri hivyo sehemu kubwa ya shughuli ya tambiko inawezesha kufikia kwa maridhiano, jambo ambalo ni muhimu kulisisitiza.

Jambo la kwanza ni kuwa mlalamikaji mwenyewe anatakiwa kuwa mwadilifu : ili tambiko lifanyike, ni lazima mlalamikaji awe tayari kwa maridhiano endapo mkosaji atajitaja na kukiri kosa. Jambo la pili ni kwenye matumizi ya vitu viwili, maziwa na mmea wa *isale* ambavyo ni ishara ya amani : ni mmea huo ambao mtaalamu wa tambiko huutumia kurushia maziwa pembeni wakati akitoa chungu katika maficho karibu na nyumba yake. Tendo hilo ni kwa ajili ya

¹¹ E. E. EVANS-PRITCHARD, 1963

kuwatuliza mizimu kwa kuwa ndiyo wao ambao hutuma majanga mbali mbali kwa watu pindi wanapochukizwa na mienendo yao. Kwa hiyo, tambiko la ‘kuvunja chungu’ lina uhusiano na imani ya kidini ambayo ni imani ya kienyeji ya Wameru iliyokuwepo kabla ya Ukristo.

Kuna mambo mengine mawili ya tambiko ambayo hulenga zaidi kupatikana kwa amani hususan katika suala la kumshinikiza mkosaji kukiri. Kwa upande mmoja ni muda wa kutosha unaotolewa hadi kufikia siku ya kufanyika kwa tambiko na kwa upande mwingine ni kwa tambiko hilo kufanyika kwa uwazi.

Tukirejea katika suala la muda wa kufanyika kwa tambiko, ni kwamba siku kadhaa hupita tangu mlalamikaji kuripoti kosa kwa mshili wa ukoo wake hadi siku ya kufanywa kwa tambiko. Muda huo hutumika kufanya majadiliano baina ya wanaukoo pamoja na kufanya uchunguzi ili kuhakikisha kuwa aliyetenda kosa siyo mmoja wa wanaukoo wao. Baada ya ukoo kufanya uamuzi, siku nyingine kadhaa hupita kabla ya kuwasilisha shauri kwa Kamati Kuu ili mchakato wa tambiko uanze. Kamati Kuu nayo kuchukua muda kujadiliana juu ya shauri husika na baada ya kufanya uamuzi, Katibu wake huandika kibali kinachoeleza ridhaa ya Kamati Kuu kuhusu kufanyika kwa tambiko. Baada ya hapo hufuata kibali kingine rasmi kutoka viongozi wa serikali za mtaa. Kibali hiki hutakiwa kuombwa na kupatikana kabla ya mlalamikaji kuoanana na mtaalamu wa tambiko. Mchakato wote huo huchukua muda. Aidha baada ya mtaalamu kukubali kufanya tambiko, maandalizi ya tambiko lenyewe nayo huchukua muda flani. Maandalizi hayo ni pamoja na

kubandika matangazo katika sehemu ambazo wakazi wengi hupita hususani maeneo ya makutano ya njia. Baada ya kuwekwa kwa tangazo hilo, kipindi rasmi cha mwezi mmoja hupita kabla ya kufanyika kwa tambiko. Mwisho, tambiko lenyewe huchukua siku kadhaa na wakati mwingine hadi juma moja. Ni wazi kuwa, muda wote huo humpa mkosaji nafasi ya kutafakari na kukiri kosa alilofanya kabla ya athari za tambiko. Hivyo, muda wote huo hulenga kutoa nafasi hiyo muhimu.

Jambo la pili ambalo ni muhimu kulisisitiza ni uwazi katika kufanyika kwa tambiko. Kwanza, habari juu ya suala hilo husambaa wakati wa majadiliano na uchunguzi ndani ya ukoo ambapo watu wengi hupata taarifa hata wale wa nje ya ukoo. Baada ya ukoo kufikia uamuzi, hatua yake ya kuomba kibali kutoka kwa Kamati Kuu nayo husambaza zaidi habari za suala hilo hususani kutokana na mjadala baina ya wajumbe wa Kamati Kuu. Kusambaa zaidi kwa habari hizo hufanywa na ubandikaji wa matangazo katika sehemu za wazi kwa kipindi cha mwezi mmoja. Tambiko lenyewe ni tendo linalofanywa na mtaalamu na hufanyika kwa kupita maeneo mbali mbali ya vijiji kwa siku kadhaa. Habari kuhusu mchakato wote huo husambaa vya kutosha na hivyo mkosaji (ambaye bado hajajulikana) hupata taarifa. Tunaweza kuchukulia kusambaa huko kwa habari kama namna ya makusudi ya kumwambia mtenda kosa : “wewe unayejificha, hivi umefikiria vya kutosha juu ya athari ambazo zitakupata? Hivi hautambui kuwa ukikiri kosa itagharimu kidogo kuliko kujificha? ”

Katika mambo mawili yaliyoelezwa awali, lile la muda na la kusambaa kwa habari za mchakato mzima, utaratibu wa tambiko la 'kuvunja chungu' unafanana na taratibu za jamii ya Ulaya kama ilivyoelezwa na Peter Brown¹² pamoja na Soazick Kerneis. Waandishi hawa wawili wanazungumzia juu ya mambo hayo mawili ambayo ni lile la muda na la kusambaa kwa taarifa katika taratibu za sheria. Kimsingi mambo hayo mawili yanachangia kuunda "chombo cha maridhiano na utaratibu maridhawa wa kukabiliana na migogoro inayoweza kuivuruga jamii"¹³. Licha ya kutofautiana kwa kiasi kikubwa kwa misingi ya maeneo na nyakati za kutumika kwake, "mifumo hii miwili ya sheria za mila zinazotegemea nguvu za mizimu" inawiana, ambapo ufanisi wa mifumo yote miwili inatokana na nguvu yake kisaikolojia na kijamii. Nguvu hiyo ni ile ile inayoonekana katika jamii nyingi na hivyo huenda mifumo kama hiyo ikawepo pia katika jamii nyingine.

Katika bara la Afrika, jamii ya Wadwala wa nchi ya Cameruni inaonekana kutumia mfumo wa sheria unaofanana na ule wa Wameru. Jambo hilo hueanda likawa na la kushangaza kutokana na jamii hizi mbili kutenganishwa na umbali wa takribani kilomita 3000. Vilevile jamii hizi mbili zina tofauti kubwa za kiisimu ingawa zote zipo katika ukanda wa lugha za Kibantu kuanzia Ghuba ya Ginnea hadi Bahari ya Hindi. Manga Bekombo-Priso¹⁴ anaeleza pia namna shauri linavyochukua muda mrefu katika mfumo wa sheria

¹² Namshukuru Soazick KERNEIS kwa kunifahamisha juu ya machapisho ya Peter BROWN.

¹³ P. BROWN, 1985, p.271-272.

¹⁴ Manga BEKOMBO-PRISO, 1995.

wa Wadwala na kwamba kamwe hakuna adhabu yoyote iliyowahi kutolewa. Anaeleza pia kwamba, kwa hakika lengo la shauri siyo kuhukumu bali kuondoa vinyongo na kurejesha mshikamano katika jamii tofauti na hukumu ambayo ingeweza kuendeleza mgogoro baina ya pande zinazovutana. Kama ilivyo kwa Wameru, kwa Wadwala pia ni mizimu ndiyo yenye dhamana ya kutoa adhabu, ambapo wakoaji huweza kukumbwa na ugonjwa ama ajali.

Dhana hizo ni tofauti na mfumo wa sheria za sasa katika jamii za Magharibi. Dhana hizi hujikita zaidi katika dhana za kidini pamoja na fikra binafsi za mhusika ambazo ni tofauti sana. Katika tambiko la Wameru, suala la mtu binafsi halina uzito sana kwa kuwa mchakato mzima hufanyika kijumuiya. Uamuzi wenyewe wa kufanya tambiko hutoka katika ukoo wa mlalamikaji hivyo ni ukoo ndiyo wenye mamlaka ya kuamua kufanyika ama kutofanyika kwa tambiko. Baada ya ridhaa ya mshili wa ukoo husika, Kamati Kuu, ambayo ni chombo cha kisiasa cha jamii nzima ndiyo huwa na dhamana ya kutoa ridhaa yake pia. Kadhalika, athari za tambiko pia ni za kijumuiya ambapo mhalifu hataadhibiwa yeye pekee bali pia familia yake na ndugu zake katika ukoo. Hatua ya tatu ambayo ni ile ya kukiri kosa na kufuta laana nayo pia hufanyika kijumuiya na ni kiongozi wa ukoo ambaye huzungumza kwa niaba ya mkosaji. “Kwa Wameru, ubinadamu ni suala la ukoo mzima na siyo suala la mtu binafsi”¹⁵. Dhana ya kuwajibika kwa mtu binafsi ambayo ni muhimu sana katika jamii za Magharibi haina umuhimu katika jamii hii.

¹⁵ Maoni ya mtoa taarifa, Jehovaroy Kaaya, Julai 2010.

Bibliografia

BAROIN Catherine, A brief history of a neo-traditional form of chieftaincy and its 'Constitution' in Northern Tanzania, 1945-2000. Dans: Wim van Binsbergen, in collaboration with Riekje Pelgrim (ed.), *The Dynamics of Power and the Rule of Law. Essays on Africa and beyond in honour of Emilie Adriaan B. van Rouveroy van Nieuwaal*, Leiden, African Studies Centre, 2003, p. 151-166.

BEKOMBO Priso Manga, Conception et exercice de la justice dans les sociétés de la côte du Cameroun, *Droit et cultures*, 29, 1995, p. 141-157.

BROWN Peter, La société et le surnaturel. Une transformation médiévale, Dans: *La société et le sacré dans l'Antiquité tardive*, Paris, Seuil, p. 265-294.

Evangelisch-Lutherische Mission zu Leipzig (éd.), *Kitabu kya isomisa vana kya Kirwa* ("Livre pour enseigner aux enfants en ki-rwa"), Leipzig, 1931.

EVANS-RICHARD Edward E., *Witchcraft, Oracles and Magic among the Azande*. London, Clarendon Press, 1963.

HARJULA Raimo, *Mirau and his practice. A study of the ethnomedicinal repertoire of a Tanzanian herbalist*. London, Tri-Med books Ltd, 1980.

KELSALL Tim, Rituals of verifications: indigenous and imported accountability in Northern Tanzania. *Africa* 73 (2), 2003, p. 174-201.

MÖHLIG Wilhelm, L'importance du serment dans la procédure judiciaire chez les Chagga du Kilimandjaro (Tanzanie). Une analyse sémantique et pratique dans une perspective historique. Dans : Verdier Raymond (ed.), *Le serment. I, Signes et fonctions*, Paris, CNRS, 1991, P. 299-313.

MUNGURE Justin E., Chungu (nungu) as a curse in traditional religion among Wameru of the ELCT – Meru Diocese, Makumira (Tanzanie), Makumira University College, 2002.